



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KILIMO  
MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO



Dar es Salaam  
31 Julai, 2024

TANGAZO KWA UMMA

**UFUNGUZI WA MSIMU WA UNUNUZI WA MBAAZI NA DENGU MWAKA 2024/2025**

Msimu wa ununuzi wa mbaazi na dengu 2024/2025 utazinduliwa rasmi tarehe 07 Agosti 2024 nchini. Mnada wa kwanza kitaifa utafanyika tarehe 07 Agosti, 2024 saa 4:00 asubuhi katika ghala la Gendi Halmashauri ya Mji wa Babati, Mkoa wa Manyara. Maeneo mengine ya Minada kwenye mikoa mbalimbali yataendelea kutangazwa kupitia tovuti pamoja na kurasa za mitandaoni za COPRA.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Sura 274. Mamlaka ya Udhhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania imetoa mwongozo wa Biashara ya zao la ufuta, mbaazi, dengu na soya Toleo la 3-2024. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine unalenga kulinda ubora wa mazao ya mbaazi, dengu, ufuta, na soya pamoja na kuongeza ushindani kupitia minada. Aidha, mwongozo huo unaelekeza utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa mbaazi na dengu kama ifuatavyo:-

- i. Mnunuzi wa mbaazi na dengu anapaswa kujisajili Mamlaka ya Udhhibiti wa Nafaka na Mchanganyiko kupitia kiunganishi <https://asds.kilimo.go.tz/register> na kuambatisha nyaraka zote muhimu zikiwemo Usajili wa Kampuni au Cheti cha Kuandikishwa (*Extract from Registrar*) kwa mfanyabiashara binafsi, Utambulisho wa Namba ya Mlipa Kodi (*TIN Certificate*), *Certificate of Tax Clearance* na Leseni ya Biashara pamoja na Namba ya NIDA;
- ii. Mnunuzi wa mbaazi na dengu anapaswa kufuata utaratibu wa uendeshaji wa minada ambayo ni ukusanyaji kupitia vyama vya ushirika, stakabadhi ghalani na mauzo ya minada ya kieletroniki yanayoendeshwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Aidha, Mwongozo wa Biashara unapatikana kwenye tovuti ya COPRA kupitia kiunganishi <https://www.copra.go.tz/publications/guidelines> ; na
- iii. Minada ya mbaazi na dengu itafanyika kila wiki katika Mikoa husika kwa kufuata ratiba itakayotolewa na kutangazwa kila wiki.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**  
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**